THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
NATIONAL EXAMINATIONS COUNCIL
CERTIFICATE OF SECONDARY EDUCATION EXAMINATION

015/2 **ELIMU YA DINI YA KIISLAMU 2**

(Kwa Watahiniwa Walioko na Wasiokuwa Shuleni)

Muda: Saa 2:30 **Jumatano, 13 Oktoba 2010 mchana**

Maelekezo

1. Karatasi hii ina sehemu A, B, C na D.
2. Jibu maswali **manne (4),** swali **moja (1)** kutoka kila sehemu.
3. Kila swali lina alama 25.
4. Vikokotozi **haviruhusiwi** katika chumba cha mtihani.
5. Simu za mkononi **haziruhusiwi** katika chumba cha mtihani.
6. Andika **Namba yako ya Mtihani** katika kila ukurasa wa kijitabu chako cha kujibia.

Karatasi hii ina kurasa 3 zenye maandishi.

Scanned by CamScanner

BISMILLAHIR - RAHMANIR - RAHIIM

SEHEMU A: QUR'AN

1. Andika tafsiri ya Surati-Fyl kisha ainisha mafunzo ya sura hii kwa muhtasari.

2. *Tuongoze njia iliyonyooka. (1:6)*
Kwa nini mwanadamu anahitaji mwongozo kutoka kwa Allah (s.w.)?

3. *Au ndio wanasema (hivi) kuwa hii (Qur'an) ameitunga (yeye mwenyewe Muhammad)? Bali wao hawaamini lolote (52:33).*
Kwa kutumia Qur'an yenyewe wathibitishie walimwengu kuwa Qur'an si kazi ya Muhammad (s.a.w).

SEHEMU B: TAWHIID

4. Toa hoja nne (4) za msingi kuonesha tofauti iliyopo baina ya Qur'an na vitabu vingine vya Mwenyezi Mungu.

5. Kwa kutumia mtazamo wa Qur'an, onesha kuwa hakuna mtu asiye na dini.

6. *Je! Haikuwabainikia tu kuwa karne ngapi tuliziangamiza kabla yao ? Na hawa (makafiri wa sasa) wanatembeatembea katika maskani yao, (hawaoni alama za kuangamizwa kwao?). Bila shaka katika hayo zimo Ishara kwa wenye akili (20:128).* Eleza mambo yanayojitokeza katika jamii ya Mtume Nuhu (a.s) yanayoonesha kuwepo kwa Allah (s.w).

SEHEMU C: FIQH

7. Bainisha viwango mbalimbali vya mali zinazojuzu kutolewa zakat kisha bainisha makundi ya watu wanaostahiki kupewa zakat.

8. Toa maelezo mafupi juu ya maneno yafuatayo:
   (a) Ihram
   (b) Talbiya
   (c) Tawaf
   (d) Sa'i
   (e) Siku za Tashirq

9. Mtume (s.a.w) Amesema : "Ndoa ni Sunnah yangu na yeyote anayekataa Sunnah yangu si pamoja nami." (*Bukhari*)
Unafikiri ni kwanini Mtume (s.a.w) amesisitiza sana kuoa ?

uk print

Scanned by CamScanner

SEHEMU D: TAREKH

10. Eleza mambo matano (5) ya awali aliyoyafanya Mtume (s.a.w) katika kuanzisha Dola ya Kiislamu Madinah.

11. Ukizingatia mafundisho yatokanayo na kazi ya Mtume (s.a.w) ya miaka kumi na tatu (13) katika mazingira ya Makka, toa darasa la namna ya kuhuisha Uislamu katika jamii yako.

12. Eleza mafunzo matano (5) tunayoyapata kutokana na historia ya Nabii Musa (a.s).

Scanned by CamScanner